**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KILIMO, BIASHARA NA UTALII YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA KAMATI KWA WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**Mheshimiwa Spika,**

Kwanza kabisa, kwa heshima na taadhima natanguliza shukrani zangu za dhati kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na utukufu kwa kutujaalia sote kuwa na afya njema na kutuwezesha kufika hapa leo kuendelea na shughuli za ujenzi wa taifa letu.

**Mhesshimiwa Spika,**

Kamati inachukuwa fursa hii kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa uongozi wake makini ambao una nia ya kuiletea nchi yetu maendeleo pamoja na wananchi wake.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu pia inatoa pongezi zake za dhati kwa Makamo wa kwanza wa Rais, Mheshimiwa Othman Masoud Othman na Makamo wa Pili wa Rais Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdallah, kwa kumshauri vyema Mheshimiwa Rais katika kutekeleza majukumu yake mazito ya kitaifa.

**Mheshimiwa Spika,**

Nitakuwa mkosefu wa fadhila iwapo sitomshukuru Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Pamoja na timu yake inayoongozwa na Katibu Mkuu, ndugu Amour Hamil Bakar kwa kusimamia vyema utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii muhimu kwa maendeleo ya taifa letu. Aidha Kamati inamshukuru kwa dhati Katibu Mkuu aliyepita Dkt. Islam Seif Salum kwa kusimamia vyema majukumu ya Wizara hii kwa kipindi chote cha uongozi wake. Tunamtakia utekelezaji mwema wa majukumu yake katika taasisi aliyohamishiwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Hata hivyo kwa namna ya pekee naomba niwapongeze wajumbe wa Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii kwa jinsi wanavyotekeleza majukumu yao ya msingi katika kuipatia Wizara hii miongozo na ushauri ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Naomba niwatambue wajumbe hao kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mheshimiwa Yussuf Hassan Idd | Mwenyekiti |
| 2. | Mheshimiwa Aza Januar Joseph | M/Mwenyeki |
| 3. | Mheshimiwa Mwanajuma Kassim Makame | Mjumbe |
| 4. | Mheshimiwa Nassor Salim Ali | Mjumbe |
| 5. | Mheshimiwa Saada Ramadhan Mwendwa | Mjumbe |
| 6. | Mheshimiwa Said Saleh Salim | Mjumbe. |
| 7. | Ndg. Mwaka Mwinyi Waziri | Katibu |

**Mheshimiwa Spika,**

Jumla ya maagizo 54 yalitolewa na Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii katika kikao cha Febuari 2022 kwa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda. Kiujumla, Kamati imeridhika na utekelezaji wa maagizo hayo na kutilia mkazo katika utekelezaji wa baadhi ya maagizo kwa maslahi makubwa ya Taifa letu kama ifuatavyo:

## JENGO KWA AJILI YA OFISI

Kamati ilipofanya ziara katika taasisi mbalimbali za Wizara hii ilibaini changamoto kubwa ya ufinyu wa ofisi katika taasisi hizo na kuishauri Wizara kufanya mpango wa kujenga jengo litakalojumuisha ofisi za Wizara hii kwa lengo la kuondosha usumbufu unaozikabili taasisi hizo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaipongeza Serikali kupitia Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa maamuzi yake sahihi ya kutaka kuzihamishia ofisi zilizo chini ya Wizara hii katika jengo la ZSTC Kinazini, hali itakayowajengea

mazingira mazuri ya kiutendaji wafanyakazi wa Wizara hii. Sote ni mashahidi kwamba mazingira bora ya kazi yanaweza kuwa chachu ya maendeleo katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku.

**Mheshimiwa Spika,**

Kupitia hali hii, Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Wizara kuharakisha ukarabati unaendelea katika jengo hilo ili kuhakikisha kwamba, taasisi zetu zinahamia kwa wakati uliokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Aidha, Kamati iliiagiza Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) kwa upande wa Pemba, kujenga jengo la Ofisi zake na Maabara kufuatia changamoto ya kukosekana kwake. Kamati inaipongeza kwa dhati Serikali kwa kuipatia Taasisi hii kiwanja katika eneo la Chamanangwe kwa lengo la kulitekeleza agizo hilo na kwamba, Wizara kupitia Taasisi hii tayari ipo katika hatua ya utayarishaji wa michoro ya ujenzi wa ofisi hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaendelea kuishauri Wizara kupitia Taasisi ya Viwango Zanzibar kuongeza kasi zaidi ya ujenzi wa ofisi hii kwa lengo la kuondokana na tatizo liliopo hivi sasa.

## MAFUNZO NA MASLAHI KWA WAFANYAKAZI

**Mheshimiwa Spika,**

Mafunzo na maslahi kwa watendaji katika taasisi zetu ni moja kati ya maagizo yaliyotolewa na kutaka kufanyiwa kazi na Wizara hii ambapo yanachukuwa nafasi ya kipekee katika kuwajengea uwezo wa kiutendaji wafanyakazi hao.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inaipongeza sana Serikali ya awamu ya nane inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa hatua aliyoichukuwa ya kuboresha maslahi ya wafanyakazi kwa kuwalipa mishahara kwa kuzingatia viwango vyao vya elimu pamoja na uzoefu wao kazini. Hali hii itasaidia sana katika kuondosha malalamiko ya watendaji yaliyopo kwa muda mrefu sasa.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika kuhakikisha kwamba, malengo ya Wizara hii yanatekelezwa kwa ufanisi mkubwa, Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Wizara kuwapatia wafanyakazi mafunzo ya muda mrefu na ya muda mfupi, mafunzo ya nadharia na vitendo kulingana na mahitaji ya taasisi zao, kwa lengo la kuwawezesha wafanyakazi hawa kwenda sambamba na mabadiliko ya sayansi na teknolojia yanayoendelea kutokea ulimwenguni kote.

## ELIMU KWA WAJASIRIAMALI

**Mheshimiwa Spika,**

Ujasiriamali ni chaguo muhimu sana katika karne hii ambapo suala hili linahitaji ujasiri na uthubutu mkubwa wa kuchukuwa maamuzi magumu hata kama kuna changamoto zinazowakabili.

Aidha, wajasiriamali walio wengi hawana ubunifu ndio sababu kubwa inayowapelekea kutofanikiwa katika harakati zao za uzalishaji.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaipongeza Serikali ya awamu ya nane kwa hatua iliyoichukukuwa yenye lengo la kuwanasua wajasiriamali kwa kuwapatia mikopo isiyo na riba kupitia benki ziliopo nchini, Mikopo hiyo itawasaidia katika kukuza na kuendeleza mitaji yao.

**Mheshimiwa Spika,**

Kupitia hali hii, Kamati inaendelea kuishauri Wizara ya Biashara kupitia taasisi husika kuendelea kutoa elimu kwa wajasiriamali juu ya fursa zilizopo nchini hivi sasa, elimu ambayo itawasaidia sana kufikia maono yao ya kuzalisha bidhaa au huduma zenye manufaa makubwa na ya uhakika kwa wateja wao.

**Mheshimiwa Spika,**

Tunaishi katika ulimwengu wa sayansi na teknolojia ambayo inaendelea kukua kwa kasi zaidi, hivyo ni vyema kwa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kuwapatia taaluma ya kutosha wajasriamali, waweze kwenda sambamba na mabadiliko hayo ili waweze kuwafikia wateja walio wengi zaidi kwa muda mfupi.

## MAENEO TENGEFU YA VIWANDA

**Mheshimiwa Spika,**

Katika kuhakikisha Tanzania inafikia uchumi wa kati, Serikali iliamua kutumia utaratibu wa kutenga maeneo maalumu kwa ajili ya ujenzi wa viwanda (Special Economic Zones) ili kurahisisha upatikanaji wa huduma zitakazowezesha uendeshaji wa viwanda hivyo. Pamoja na kutengwa kwa maeneo hayo, bado yanakabiliwa na changamoto za hapa na pale kama vile ukosefu wa miundombinu ya barabara za kuelekea katika maeneo husika na miundombinu ya maji, hali ambayo inaweza kuwa kikwazo kwa wawekezaji.

**Mheshimiwa Spika,**

Uzoefu unaonesha kwamba, maeneo mengi ya uwekezaji yanaendelea kuvamiwa na wananchi wanaoishi karibu na maeneo hayo, hii ni kwa sababu maeneo hayo bado hayajadhibitiwa hali inayotoa fursa kwa wananchi kuyatumia maeneo hayo kwa shughuli mbalimbali za kijamii ikiwa ni pamoja na kilimo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kutokana na umuhimu wa maeneo hayo, Kamati inaendelea kuishauri Wizara kupitia Idara ya Maendeleo ya Viwanda kuongeza mashirikiano ya karibu na jamii iliyozunguka maeneo hayo kwa lengo la kuyahifadhi na kuepusha migogoro inayoweza kutokea ili miradi iliyokusudiwa iweze kukamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,**

Aidha, Kamati inaipongeza Wizara ya Biashara kwa kuendelea na ujenzi wa viwanda katika eneo la uwekezaji Chamanangwe kisiwani Pemba, ambapo kukamilika kwa ujenzi wa viwanda hivyo kutaibua fursa kubwa ya ajira kwa vijana wetu. Viwanda kadhaa vinatarajiwa kujengwa ikiwa ni pamoja na kiwanda cha maji safi na salama (Amos Industial Ltd), ambacho kwa sasa tayari kimenza uzalishaji wake.

## USIMAMIZI WA MIFUMO YA TEHAMA - SMIDA

**Mheshimiwa Spika,**

Mifumo ya TEHAMA ni muhimu sana katika utekelezaji wa majukumu ya taasisi zetu kwani inasaidia katika kuleta ufanisi wa utekelezaji wa majukumu sambamba na kurahishisha upatikanaji wa takwimu halisi katika taasisi zetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kuhakikisha kwamba kitengo cha TEHAMA cha Wizara kinashirikiana kwa karibu na Serikali -Mtandao (E-Government) kwa lengo la kuusimamia mfumo huu uweze kukamilika na kuweza kutumika katika kutekeleza shughuli za Wizara kwa ufanisi.

## KUITANGAZA CHAPA YA BIDHAA ZA ZANZIBAR (BRAND OF ZANZIBAR)

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imeridhika na utekelezaji wa agizo ambalo liliitaka Wizara kupitia Idara ya Maendeleo ya Viwanda kuitangaza ***Brand*** yetu ndani na nje ya nchi kupitia bidhaa mbalimbali zinazoingia sokoni kwa mauzo.

**Mheshimiwa Spika,**

Wajasiriamali wanahitaji uelewa mkubwa juu ya umuhiumu wa kuitumia brand hii kwa bidhaa wanazozizalisha

Kwa muktadha huo Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kuendelea kutoa elimu kwa wajasiriamali na wafanya biashara wote kwa ujumla kuhakikisha wanaitangaza ***brand*** hii kupitia biashara zao na wananchi nao kwa upande wao kununua bidhaa zenye ***brand*** ya Zanzibar. Hali hii itaweza kuzitangaza bidhaa zinazozalishwa nchini kwa kasi zaidi.

## UKODISHWAJI WA VIWANDA

**Mheshimiwa Spika,**

Kufuatia agizo la Kamati kwa Wizara ya Biashara juu ya kukiwezesha kiwanda cha Makonyo kisiwani Pemba kuzalisha bidhaa zilizo bora zaidi

kwa lengo la kujitangaza kitaifa na kimataifa, Kamati ilipokea taarifa ya kwamba, kiwanda hicho kwa sasa kinajiendesha kwa hasara, hasa tukizingatia uzalishaji wa mafuta ya makonyo kiwandani hapo ni wa gharama kubwa na tija inayopatikana ni ndogo mno.

**Mheshimiwa Spika,**

Kupitia hali hii, Wizara ina lengo la kukikodisha kiwanda hiki ambapo kwa sasa tayari wapo wawekezaji ambao wemeonesha nia ya kutaka kuwekeza katika kiwanda hiki.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inatoa rai kwa Serikali kupitia Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, kabla ya kuchukua maamuzi ya kukikodisha kiwanda hiki, basi ni vyema kwanza Wizara ikafanya upembuzi yakinifu juu ya umuhimu, faida na hasara ya kuwepo kwa kiwanda hiki nchini. Endapo Serikali itaamua kukikodisha kiwanda hiki, ni vyema kwa Wizara kupitia Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) kuisimamia ipasavyo mikataba ya ukodishwaji wa kiwanda hiki kwa lengo la kuepusha migogoro baina ya Serikali na muwekezaji huyo hapo baadae.

## KUBAKISHA MAKUSANYO (RETENTION) KWA ZBS NA ZFCC

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ilitoa ushauri kwa Serikali kwa zile taasisi zinazokusanya mapato kuwaruhusu kubakisha fungu la fedha hizo japo kwa asilimia ndogo na kuruhusiwa kuzitumia katika utatuzi wa baadhi ya changamoto zinazojitokea katika taasisi hizo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kufuatia hali hii, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kwamba taasisi hizi ziruhusiwe kubakisha fedha za makusanyo hayo ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa . Kamati imebaini kwamba kuna baadhi ya changamoto zinakwama utekelezaji wake, sababu kubwa ni kwa taasisi hizo kukaa na kusubiri fungu la OC pekee, endapo fedha hii itakuwepo itaweza kuziba pengo hilo na hatimae maendeleo endelevu yanaweza kupatikana katika taasisi zetu.

## UHAKIKI WA BIDHAA KUTOKA NJE YA NCHI

**Mheshimiwa Spika,**

Wakala wa Vipimo Zanzibar (ZAWEMA) ni taasisi muhimu sana yenye lengo la kukidhi matakwa ya Serikali na jamii, kwa upande wa usimamizi wa kumlinda mlaji dhidi ya matumizi yasiyo sahihi ya vipimo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kufuatia maoni na ushauri wa Kamati kwa Wakala wa Vipimo Zanzibar wa kuzipima bidhaa zote zinazozalishwa nje ya nchi, Kamati inaendelea kuishauri Wizara kupitia taasisi hii kuharakisha zoezi hili kutokana na umuhimu wake. Kufanikiwa kwa upimaji wa bidhaa hizi kutaweza kutanua wigo kwa taifa letu na taasisi za kikanda na za kimataifa katika masuala ya vipimo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati pia inaishauri Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kupitia Taasisi hii, kutoa elimu na ushauri wa kitaalamu kuhusu masuala ya vipimo kwa wadau nchini, kuongeza na kutanua wigo wa kazi za vipimo kwa maeneo mapya ambayo kwa sasa bado hayajafikiwa. Aidha,Wakala iendelee kutoa elimu hii kwa jamii kuachana na tabia ya kutumia vipimo batili kama vile ndoo, dumu, makopo, na badala yake watumie mizani sahihi ambazo zimehakikiwa na Wakala wa Vipimo, kufanya hivyo kutasaidia kujenga uaminifu zaidi katika biashara zao.

## HITIMISHO

Mwisho kabisa, napenda kukushukuru wewe binafsi **Mheshimiwa Spika,** kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati yangu kwa niaba ya Kamati, pamoja na kuwashukuru wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kumega wakati wao na kunisikiliza kwa umakini mkubwa wakati nikiwasilisha hutuba hii. Sasa wakati umefika niwaombe wajumbe wa Baraza lako waijadili na kuichangia hotuba hii kwa mustakbali wa taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,**

Mimi binafsi na kwa niaba ya Kamati ninayoiongoza naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**Mheshimiwa Spika,**

Baada ya maelezo hayo, naomba kuwasilisha.

**Ahsante,**

…………………………….

Mhe.Yussuf Hassan Idd.
Mwenyekiti,
Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii
Baraza la Wawakilishi
**Zanzibar.**